# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 009 SEPTEMBA 2021

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



## 1 TMA, WADAU WA MADINI WAKUTANA

## 2 VIFAA VIPYA VYA HALI YA HEWA VYA KUPIMA ANGA LA JUU VYASIMIKWA JNIA



## 3 SALAMU ZA PONGEZI: WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI



**KITAIFA**

# TMA, WADAU WA MADINI WAKUTANA

**Dodoma**



TMA imekutana na wadau wa sekta ya madini nchini ili kujenga uelewa wa pamoja wa utekelezaji wa Kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na.2 ya 2019. Mkutano huo ulifanyika katika ukumbi wa PSSSF (Makale), Dodoma, Tarehe 29 - 30 Septemba 2021. Akizungumza wakati akifungua mkutano wa Wadau wa Madini mgeni rasmi, ambaye ni mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Bw. Hamid Mbegu alisema kanuni hizo zimekamilika na zipo tayari kwa utekelezaji.

“Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imekamilisha kanuni saba za sheria Na.2 ya 2019. Utekelezaji wa kanuni hizi katika sekta ya madini utasaidia kupunguza madhara yanayotokana na matukio ya hali ya hewa migodini kupitia matumizi ya taarifa mahsusi na sahihi za hali ya hewa”. Alizungumza Bw. Mbegu.

Aidha, Bw. Mbegu alisema TMA imeandaa mifumo ya kufungasha na kufikisha huduma kwa wadau wa sekta ya madini sambamba na mfumo wa kusajili vituo vyahali ya hewa nchini kwa kuzingatia masharti ya kanuni juu ya uwekaji na uendeshaji wa vituo vya hali ya hewa ili kupata takwimu sahihi kwa matumizi

mapana ya sekta ya hali ya hewa na wadau wake.

Awali, wakati akimkaribisha mgeni rasmi, Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) alieleza jukumu la Mamlaka ya Hali ya Hewa na umuhimu wa kikao hicho cha wadau wa madini.

“Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ina jukumu la kuhakikisha inatoa huduma za hali ya hewa zilizo bora kwa wadau mbalimbali ikiwepo sekta ya madini. Hivyo, kikao hiki ni muhimu kwasababu kitagusa maeneo mawili muhimu ya kisheria na tayari yapo katika kanuni, ambayo ni umiliki wa vituo vya hali ya hewa na uchangiaji wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika sekta ya madini nchini”. Alisema Dkt. Kijazi.

Kwa upande wa wadau, waliishukuru TMA kwa ushirikishwaji wa mkutano huu wa kujenga uelewa wa pamoja wa utekelezaji wa kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na.2 ya 2019 na kusema matumizi ya taarifa za hali ya hewa katika sekta ya madini ni muhimu hivyo Mamlaka itoe elimu zaidi ili kupata uelewa wa pamoja kwa wadau wote.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Adv. Mohamed Salum akizungumza wakati wa kufunga mkutano huo, aliwashukuru wadau wa sekta ya madini kwa kushiriki mkutano huo wa kujenga uelewa wa utekelezaji wa kanuni za TMA zilizokuwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na.2 ya 2019 na kukiri kuwa wadau wameonesha uelewa mkubwa na umuhimu juu ya utekelezaji wa sheria hii na namna itakavyowasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ya uchimbaji wa madini na kuonesha kwamba uhitaji wa taarifa za hali ya hewa ni jambo la muhimu kabla ya kuanza shughuli zao.



KIMATAIFA

# VIFAA VIPYA VYA HALI YA HEWA VYA KUPIMA ANGA LA JUU VYASIMIKWA JNIA

**Dar es Salaam**



Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) limeipatia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) vifaa vipya vya kupima hali ya hewa ya anga la juu (upper air).Vifaa hivyo vimetolewa kwa TMA ikiwa ni msaada chini ya utekelezaji wa program ya WMO ya kuboresha huduma za hali ya hewa kwa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki (EAC) zinazozunguka eneo la Ziwa Viktoria, iitwayo "**HIGH impact Weather lAke SYstems (HIGHWAY)**".

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na: mtambo wa kuzalisha gesi ya haidrojeni (Hydrogen gas Generator); radiosonde; Maputo

maalumu ya kupima hali ya hewa ya anga za juu (weather balloons);program za kompyuta (computer softwares)na mavazi maalumu kwa ajili ya usalama. Vifaa hivyo vimefungwa tarehe 7 Septemba, 2021 katika kituo cha kupima hali ya hewa ya anga la juu (Upper Air Station) kilichopo katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam (JNIA).



Aidha, zoezi la ufungaji wa vifaa hivyo lilienda sambamba na mafunzo kwa wataalamu.

Ufungwaji wa vifaa hivyo umewezesha kuhuisha kituo hichokuwa cha kisasa zaidi baada ya mitambo ya awali kuwa chakavu. Kituo hicho kwa sasa kitaendelea na shughuli zake za kupima hali ya hewa ya anga la juu kama kawaida.Uhuishaji wakituo hicho utawezesha kupima takwimu za hali ya hewa ya anga la juu, ambazo ni muhimusanakatikakutoautabiri wa hali ya hewa kwa matumizi mbalimbali hususan usalama na usafiri wa anga nchini.

Programu hiyo ya HIGHWAY ilitekelezwa nchini Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia Septemba, 2017, ambapo miongoni mwa shughuli zake zilihusisha pia uhuishaji wa kituo hicho cha kupima hali ya hewa ya anga la juu katika uwanja wa JNIA. Msaada wa vifaa vilivyotolewa na WMO ni sehemu ya utaratibu wa Shirika hilo ikiwa ni mrejesho kwa Nchi Wanachama kutokana na michangoinayotolewanaSerikali za Nchi Wanachama kupitia ada ya uanachama kwa Shirika hilo.

# SALAMU ZA PONGEZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**



## PONGEZI

**MHE. PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB)**

Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), tunakupongeza kwa kuteuliwa na kuapishwa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**HONGERA SANA**

*Hali ya Hewa kwa Maendeleo Endelevu*

@tmaservices @tma_services @tanzaniameteorological

tanzaniametagency www.meteotz1950.blogspot.com TMAonline TV

# KISWAHILI CHETU

## ISTILAHI ZA HALI YA HEWA

Tuangazie herufi I:

| | |
|---|---|
| immune system | mfumokinga |
| imported transmission | maambukizi kutoka nje |
| incubation period of COVID 19 | kipindi cha upevukaji cha UVIKO -19 |
| incubation period | kipindi cha upevukaji |
| infection | maambukizo |
| infection control | udhibiti wa maambukizo |
| infectious diseases | magonjwa ya kuambukiza |
| isolate | tenga |
| isolation | utengaji |
| isopropyl alcohol | alkoholi isopropili |


JARIDA LA MWEZI
AGOSTI, 2021
TOLEO NA. 008
1 BODI YAWATAKA WADAU WA HALI YA HEWA KUTOA USHIRIKIANO MZURI KWA TMA
2 DKT. KIJAZI AELEZA FAIDA KWA NCHI WANACHAMA WA WMO KANDA YA AFRIKA
3 FAHAMU ZAIDI: MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA HALI MBAYA YA HEWA WA SIKU TANO


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Kennedy Mgeta
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa
Kituo Kikuu cha Utabiri



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV

Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
388 Br. Morogoro
S.L.P 3056,
16102 Dar es Salaam, Tanzania.